**kwa sababu ya roho hizi vuguvugu. Ni wao waliosababisha nilie; Baba ikiwa ni mapenzi yako uniondolee mbali kikombe hiki nisikinywe. Kwa watu hawa, tumaini la mwisho lililowabakia ni kuikimbilia Huruma yangu tu basi."**

Ee Yesu mwenye Huruma nyingi, Wewe u Huruma yenyewe. Nazileta roho vuguvugu kwenye Moyo wako ulio na Huruma. Roho hizi ni kama mizoga iliyojaa na kunuka uvundo, uziingize katika moto wa upendo wako safi, zitakasike. Roho hizi zilikutia machukizo mengi. Sasa uziangaze tena kwa Huruma yako, uzipe paji la Upendo Mtakatifu. Ee Yesu mwenye Huruma Kuu, tumia uwezo wako uzipatie roho hizi bidii tena, kwani kwako hakuna kitu kisichowezekana. Baba wa Huruma, uzitazame kwa macho ya Huruma, roho zilizo vuguvugu, ambazo katika hali yao hiyo, wamefungamanishwa na Moyo wa Mwanao Yesu, ulio kilindi cha Huruma. Ee Baba wa Huruma, tunakusihi kwa ajili ya mateso makali ya Mwanao Mpenzi, Bwana wetu Yesu Kristo, uliyovumilia pale msalabani, kwa masaa matatu ukiwa katika hali ya umahututi na uchungu, uziwezeshe roho hizi zisifu utukufu wa huruma yako. *Amina.*

Wakati unapoenda kuungama, kwenye chemichemi hii ya huruma, damu na maji zilizobubujika toka ndani ya Moyo wangu, daima hutiririka juu ya roho yako... Katika Mahakama ya Huruma [*sakramenti ya Upatanisho*]... miujiza mikubwa hufanyika tena na tena... Hapa mahangaiko ya nafsi hukutana na Mungu wa Huruma...

Njoo kwa imani miguuni pa mwakilishi wangu... Mimi mwenyewe nasubiri hapo kwa ajili yako. Nimefichwa tu na Kuhani... Mimi mwenyewe hutenda ndani ya nafsi yako... Fanya Ungamo lako mbele yangu. Nafsi ya Kuhani ni, kwa ajili Yangu, ni kama pazia tu. Usijiulize ni Kuhani wa aina gani ninayemtumia kwa kazi yangu; fungua nafsi yako na ungama kana kwamba ungeungama kwangu, nami nitaijaza kwa mwanga wangu...

Roho zingekuwa kama miili inayooza, kwa mtizamo wa kibinadamu, kusingekuwa na matumaini ya marejesho kwani kila kitu kingekuwa tayari kupotea, si hivyo kwa Mungu. Muujiza wa Huruma ya Kimungu unarejesha roho hiyo kwa ukamilifu... Kutoka kwenye chemchemi hii ya huruma, roho huchota neema kwa kipimo cha uaminifu. Ikiwa uaminifu wao ni mkubwa, hamna kikomo kwa ukarimu wangu.

Bwana wetu amefanya kupokea Ekaristi na Upatanisho kuwa muhimu kwa ajili ya kupokea ahadi yake ya msamaha kamili wa dhambi na adhabu kwa wale wanaoshika sikukuu ya huruma. Na Papa Yohane Paulo II, ambaye kwa kurudia alisisitiza umuhimu wa ujumbe wa Mungu wa huruma, ametuhimiza kwamba, "Kanisa la Ujio mpya... lazima kuwa Kanisa la Ekaristi na Toba." (*Redemptor hominis*)

## SALA YA MAJITOLEO KWA HURUMA YA MUNGU

Yesu, Huruma ya Mungu, kuanzia leo, nayatolea maisha yangu yote kwako bila kujibakiza. Nayaacha Mikononi mwako mambo yangu ya zamani, ya sasa, na ya baadaye. Tangu leo na kuendelea, nifanye niwe mfuasi wa kweli wa Mafundisho yako. Fanya Picha ya Huruma ya Mungu, ilinde nyumba yangu na familia yangu dhidi ya nguvu zote za uovu katika ulimwengu huu wa leo. Naomba wote wanaoiheshimu wasiangamie kamwe, bali iwe furaha maishani mwao, tumaini lao katika kifo, na utukufu wao milele. *Amina.*

## KUOMBA HURUMA YA MUNGU KWA WATOTO WASIOZALIWA

Kwa wale wote wasio na msaada, watoto wadogo wanaokufa tumboni mwa mama zao, ninaomba kwamba roho hizi zote ndogo zipewe uzima wa milele na Bwana wetu, Yesu Kristo, kupitia Huruma yake ya Kimungu na ninamwomba Yesu aonyeshe huruma yake kwa wazazi wa watoto hawa, haswa kwa akina mama, ambao hawajui wanalofanya. Bwana, uwaangazie na uwape ufahamu wa kina juu ya thamani na uzuri wa maisha. Kwa Huruma yako usamehe machungu yote waliyoyasababisha na uwaonyeshe njia ya uzima wa milele. *Amina.*

## ROZARI YA HURUMA YA MUNGU

### SALA YA KUANZIA

Yesu, wewe uliyezimika, lakini chanzo cha uhai kilitoka kwa ajili ya roho, na bahari ya huruma ilifunguka kwa ajili ya ulimwengu mzima. Ee Chemchemi ya Uhai, Huruma isiyoelezeka, iliyofunika ulimwengu wote na ukajitoa kwetu sisi. Ee Damu na Maji, zilizobubujika toka Moyoni kwa Yesu kama chemchemi ya huruma kwetu. Ninakutumainia!

**1. Anza kwa:**
- Ishara ya Msalaba
- Baba yetu moja
- Salamu Maria moja
- Kanuni ya Imani ya Mitume

**2. Kisha kila penye punje kubwa sali sala hii:** Baba wa Milele, ninakutolea Mwili na Damu, Roho na Umungu, wa Mwanao Mpenzi sana, Bwana wetu Yesu Kristo, kwa kulipia dhambi zetu, na dhambi za ulimwengu mzima.

**3. Penye punje 10 utasali (badala ya Salamu Maria):** Kwa ajili ya mateso makali ya Bwana wetu Yesu Kristo, Utuhurumie sisi na ulimwengu mzima.

(*Rudia hatua ya 2 na ya 3 kwa mafungu yote matano*)

**4. Hitimisha na (mara tatu):** Mungu Mtakatifu, Mtakatifu mwenye Enzi, Mtakatifu unayeishi milele, Utuhurumie sisi na ulimwengu mzima.

### SALA YA KUFUNGA

Mungu wa milele, huruma yako haina mwisho na ni hazina isiyokauka. Ututazame sisi na kutujalia huruma yako, ili kwamba tunapokutana na magumu, tusikate tamaa wala kuhuzunika, bali kwa imani dhabiti tujiweke chini ya mapenzi yako Matakatifu, ambayo ndiyo upendo na huruma yenyewe. *Amina.*

Sala.land




*Anza kila siku kwa kusali Rozari ya Huruma ya Mungu kisha Sali nia ya siku husika:*

## SIKU YA KWANZA 1

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee wanadamu wote, na hasa wakosefu. Uwazamishe ndani ya Bahari Kuu ya Huruma yangu. Kwa njia hii utatuliza uchungu wangu kwa ajili ya roho zilizopotea."**

Ee Yesu mwenye huruma, ambaye asili yako ni huruma na msamaha, usizitazame dhambi zetu, bali utazame tumaini tulilo nalo katika wema wako usio na mwisho. Utupokee sisi sote chini ya ulinzi wa moyo wako wenye huruma tele. Usimwache hata mmoja. Tunakuomba hayo kwa njia ya upendo ule unaokuunganisha wewe na Baba na Roho Mtakatifu. Baba wa Milele, uwatazame kwa macho ya huruma wanadamu wote, na hasa wakosefu maskini, waliofunikwa ndani ya Moyo wa Mwanao mpenzi, Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa ajili ya mateso makali ya Yesu, utuoneshe huruma yako, ili nasi tuisifu na kuitukuza, tangu sasa na milele yote. *Amina.*

## SIKU YA PILI 2

**Maneno Mwokozi wetu: "Leo niletee roho za makuhani na watawa, uwazamishe katika kilindi cha huruma yangu isiyo na mwisho. Ni wao hasa walionipa nguvu ya kuweza kuyavumilia mateso yangu makali mno. Kwa njia yao, kama vile mifereji, huruma yangu humiminika na kuwatiririkia binadamu wote."**

Ee Yesu mwenye huruma tele, kwako hutoka mema yote. Uwazidishie neema yako waume kwa wake waliojitolea na kuwekwa wakfu katika utumishi wako, ili watekeleze utumishi wao kwa huruma na kwa jinsi inayofaa, na kwamba wale wanaowaona na kuzishuhudia kazi zao bora, waweze kumtukuza Baba wa Huruma aliye mbinguni. Baba wa Milele, uwazame kwa huruma, jeshi teule la wafanyakazi shambani mwako. Uzitazame kwa wema roho zao mapadre na watawa wote. Uwajalie wingi wa baraka zako. Kwa njia ya upendo wa Moyo wa Mwanao waliofungamanishwa nao, uwape nguvu na mwanga, ili waweze kuwaongoza wengine katika njia ya wokovu, na kwa sauti moja, waihimidi huruma yako kwa nyimbo za sifa bila mwisho. *Amina.*

## SIKU YA TATU 3

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee roho za watu wenye uaminifu na uchaji wa Mungu, na uwazamishe katika Bahari Kuu ya Huruma yangu. Roho za watu hawa ndizo zilizonifariji katika njia ya Msalaba. Wao ndio waliokuwa tone lile la faraja nilipokuwa katikati ya bahari ya uchungu na mateso."**

Ee Yesu mpole na mwenye huruma sana, Wewe huchota neema kwa wingi kutoka katika hazina Yako, na kuzigawa kwa ukarimu kwa kila mmoja wetu na kwa watu wote. Tunakuomba utupokee katika makao ya Moyo wako mpole na wenye huruma nyingi, na usituache tujitenge nawe kamwe. Tunakuomba neema hii, kwa ajili ya mapendo ya ajabu, yawakayo moyoni mwako kwa Baba yako wa mbinguni. Baba wa Milele, elekeza uso wako wa huruma, kwa watu wote walio waaminifu, kama vile kwenye hazina na urithi wa Mwanao. Kwa ajili ya mateso yake ya kuhuzunisha, uwajalie Baraka zako, na ulinzi wako daima. Kwa njia hii, waweze kuimarika katika upendo, na wala wasije wakapoteza hazina bora ya Imani Takatifu, bali, pamoja na majeshi yote ya Malaika na Watakatifu, waweze kuisifu na kuitukuza huruma yako isiyo na mwisho, kwa milele yote. *Amina.*

## SIKU YA NNE 4

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee wale wote wasioniamini na wale wasionijua bado. Wao pia niliwafikiria wakati wa mateso yangu makali, na juhudi watakayokuwa nayo baadaye ilinituliza Moyo wangu. Uwaingize katika Bahari Kuu ya Huruma Yangu."**

Ee Yesu mwingi wa Huruma, Wewe ni Mwanga wa dunia nzima. Uzipokee katika makao ya Moyo wako wenye huruma sana, roho za wale wote wasiokuamini na wale wasiokujua bado. Achia mionzi ya neema yako iwaangazie, ili nao, pamoja nasi sote, tuitukuze huruma yako ya ajabu, na usiwaache wajitenge na makao hayo, ambayo ni Moyo wako uliojaa huruma. Baba wa Milele, uzitazame kwa huruma yako, roho za watu wale wasiomwamini Mwanao, na za wale ambao hawajakujua bado, lakini wamefungamanishwa ndani ya Moyo wa Yesu uliojaa huruma tele. Uwavute kwenye mwanga wa Injili. Hawa hawajajua Ukuu wa furaha iliyopo katika kukupenda Wewe. Uwajalie nao pia waweze kuitukuza hisani ya huruma yako kwa milele yote. *Amina.*

## SIKU YA TANO 5

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee roho za ndugu waliojitenga na Kanisa, na uwazamishe katika Bahari Kuu ya Huruma yangu. Wakati ule wa mateso yangu makali, watu hawa waliurarua mwili wangu na Moyo wangu, yaani Kanisa langu. Pindi warudipo tena katika Umoja wa Kanisa, majeraha yangu hupona, na kwa njia hii wanapunguza ukali wa mateso yangu."**

Ee Yesu Mpole na mwenye Huruma, Wewe ndiwe Wema wenyewe, hukatai kuwapa mwanga wale wote wanaoutafuta. Uzipokee ndani ya Moyo wako wenye Huruma, roho za ndugu zetu waliojitenga. Uwavute kwa mwanga wako, ili warudi tena katika Umoja wa Kanisa lako Takatifu, na uwadumishe humo, wasijitenge tena na Moyo wako wa Huruma, bali uwawezeshe wao pamoja nasi, kuusifu na kuutukuza ukarimu wa Huruma Yako. Baba wa Milele, uzitazame kwa huruma, roho za ndugu zetu waliojitenga na Kanisa lako Takatifu, hasa wale waliozitapanya Baraka zako na kuzitumia vibaya neema zako, kwa kuendelea kushupaa katika mafundisho yao ya upotofu. Usiyaangalie hayo makosa yao, bali uutazame upendo wa Mwanao Mpenzi, pamoja na mateso yake makali aliyovumilia kwa ajili yao. Watu hawa pia, wamefungamanishwa na Moyo wa Mwanao Yesu, wenye Huruma Kuu. Uwawezeshe wao pamoja na sisi sote, tuisifu na kuitukuza Huruma Yako Kuu, kwa milele na milele. *Amina.*

## SIKU YA SITA 6

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee roho za watu walio wapole na wanyenyekevu wa moyo, pamoja na roho za watoto wadogo, na uzizamishe katika kilindi cha Huruma yangu. Roho hizi hufanana kwa ukaribu zaidi na Moyo wangu. Hawa ndio walionitia nguvu wakati wa mateso na uchungu wa mahututi yangu. Niliwaona kama malaika wa duniani, ambao watakesha daima kuabudu katika altare zangu. Hawa nitawamwagia neema zangu zote. Kwa maana ni roho ile tu iliyo na unyenyekevu inaweza kupata neema zangu. Ninapendelea na kuziamini sana roho nyenyekevu."**

Ee Yesu mwenye Huruma sana, Wewe Mwenyewe ulisema: "Jifunzeni kwangu kwa maana Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa Moyo." Uwapokee ndani ya Moyo wako uliojaa Huruma, watu wote walio wapole na wanyenyekevu, pamoja na roho za watoto wadogo. Roho hizi hustaajabisha Mbingu nzima, maana wanapotokea mbele ya Kiti cha Enzi cha Baba wa mbinguni, huwa kama shada la maua litoalo harufu tamu ya marhamu safi, na kuifurahisha Mbingu nzima. Mungu Mwenyewe hufurahia manukato yao safi. Ee Yesu, Roho hizi zina makao ya daima ndani ya Moyo wako wenye Huruma. Na daima hukuimbia wimbo wa Huruma na Upendo wako. Baba wa Milele, uzitazame kwa Huruma, roho za watu wote walio wapole na wanyenyekevu wa moyo, pamoja na roho za watoto wadogo, waliofungamanishwa na Moyo wa Huruma ya Yesu Mpenzi. Roho za watu hawa, hufanana na Mwanao kwa karibu zaidi. Harufu yao tamu ya fadhila hukufurahisha sana, nayo hupanda ikianzia hapa duniani mpaka kwenye Kiti chako Kitukufu. Ee Baba wa Huruma na wema wote, ninakuomba, kwa ule upendo ulio nao kwa roho hizi penzi, na kwa ajili ya furaha uipatayo kwao, utubariki sisi na ulimwengu mzima, ili sote pamoja tuungane katika kuisifu Huruma Yako, kwa milele yote. *Amina.*

## SIKU YA SABA 7

**Maneno ya Mowokozi wetu: "Leo niletee roho za wale ambao kwa namna ya pekee huiheshimu na kuitukuza Huruma yangu, na uwazamishe ndani ya Huruma Yangu. Roho hizi ndizo zilizonisikitikia zaidi wakati wa mateso yangu na kuipenya kabisa roho yangu. Hawa ndio vielelezo na sura halisi ya Moyo wangu wenye Huruma na Wema. Roho hizi zitakuja kung'aa kwa namna ya pekee katika maisha ya milele ijayo. Hakuna hata mmoja kati yao atakayetupwa katika moto wa milele. Mimi Mwenyewe nitamkinga kwa namna ya pekee kila mmoja wao saa ile ya kufa kwao."**

Ee Yesu mwenye Huruma, Moyo ulio Upendo wenyewe, uzipokee ndani ya Moyo wako wenye Huruma sana, roho za watu wale wanaoheshimu na kutukuza kwa namna ya pekee Ukuu wa Huruma yako. Roho hizi hushinda kwa nguvu ya Mungu mwenyewe. Hukazana kihodari, hata katikati ya taabu na dhiki za kila aina, wakiitumainia tu Huruma Yako, na kwa kujiunga nawe, ee Yesu, huwabeba wanadamu wote mabegani mwako. Roho hizi hazitahukumiwa vikali, bali Huruma Yako itazikumbatia pindi ziondokapo kwenye maisha haya. Baba wa Milele, uzitazame kwa Huruma, roho za watu wale ambao kwa juhudi na upendo wa pekee, huitukuza na kuiheshimu Huruma yako isiyo na mipaka, ambao wamefungamanishwa ndani ya Moyo wa Yesu ulio na Huruma tele. Watu hawa ni kama Injili iliyo hai. Wanakutukuza kwa maneno na matendo yao, na kwa kukuiga Wewe, huwatendea watu wenzao kwa wema na huruma. Tunakuomba uwaonyeshe Huruma yako Kuu zaidi na zaidi, kadri ya tumaini lao kwako na kwa ahadi zako. Mwanao Yesu Kristo Mwenyewe atawaleta kama utukufu wake, tangu wakati huu wakiwa bado hapa duniani. Lakini hasa saa yao ya kufa. *Amina.*

## SIKU YA NANE 8

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee roho za wale waliofungwa bado toharani, na uwazamishe ndani ya Bahari Kuu ya Huruma yangu. Humo, mafuriko ya Damu yangu, yazimishe miali ya moto mkubwa unaowachoma. Roho hizi zote hupendwa sana nami. Wako humo toharani kwa ajili ya kulipia Haki yangu waliyoikosa hapa duniani. Wewe una uwezo wa kuwapatia faraja. Chota rehema zote za Kanisa langu na uzitolee kwa ajili yao. Ungalijua tu ukali wa mateso yao, loo! Ungetolea daima sadaka za kiroho kwa ajili yao, na kulipa deni zima la Haki ya Mungu."**

Ee Yesu mwenye Huruma, wewe mwenyewe umesema wataka rehema; Uzitazame kwa Huruma roho zile zinazoteswa toharani, kwa kulipia deni la Haki ya Mungu waliyoikosea. Mtiririko ule wa Damu na Maji uliotoka kwa kasi Moyoni mwako, uzimishe miale ya moto mkali wa toharani, ili huko pia Huruma yako isifiwe na kuadhimishwa. Baba wa Milele, uzitazame kwa wema na Huruma, roho zile zinazoteswa Toharani, wao pia wamefungamanishwa ndani ya Moyo wa Mwanao Mpenzi Yesu, na uchungu wote ulioelemea Moyo na Roho yake, onyesha Huruma yako kwa roho zilizotiwa nguvuni na Haki yako. Uwatazame watu hao kwa njia ya Madonda yake Yesu Mwanao Mpenzi, kwa kuwa tunaamini kabisa kuwa wema na Huruma yako havina mwisho. *Amina.*

## SIKU YA TISA 9

**Maneno ya Mwokozi wetu: "Leo niletee roho za wale waliokwishaingia hali ya uvuguvugu, na uwazamishe katika kilindi cha Huruma yangu. Roho hizi huumiza sana Moyo wangu. Nafsi yangu iliteseka sana katika Bustani ya Mizeituni**